# KILA ALIYEMWAMINI YESU MBELE YAKE (ANAYO MASHINDANO ANAYO MITIHANI YA KUFANYA ILI AWE MSHINDI)
# MAANDIKO: EBR 12:1-4 (EBR 10:23, 38-39)

1. Mashujaa wa imani katika sura ya 11 ya kitabu cha Ebrania ambao ndiyo mwandishi anawataja kama mashahidi wanaotuzunguka sisi watakatifu wa leo ambao tumemwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wetu; watakatifu hawa waaminifu wa Mungu walikataa kata kata kuishi maisha ya kuendekeza tamaa za mwili huu, au tama za macho ikiwa ni pamoja nakukataa starehe zote mbaya na za kipagani (yaani **waliikata** dunia hii kabisa jambo lililoifanya dunia nayo iwakatae) ***Ebr. 11:38***

- Kabla ya kuifikia heshima hii ya kutajwa kama mashahidi mbele za Mungu kwa ajili ya ndugu zao ambao bado tuko duniani **tukimenyana** na adui baada ya kuokoka; wao pia walishindana na adui na baada ya kushinda ndipo mbingu zinawaweka kama mashahidi ili kusudi watu wengine watakaoshindwa wasipate nafasi ya kujitetea mbele za Mungu siku ile ya hukumu

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia tunapokuwa katika mashindano haya (tunapokuwa tunakutana na mitihani mbalimbali katika safari yetu hii ya kwenda nchi ya ahadi (Mbinguni)**

a. **Ni kuhakikisha kabisa kwamba UNGAMO letu haligeuki /halibadiliki** ***Kumb. 29:9, 1Timoth 6:12-14, Ebr. 3:1, 4:14, 10:23***

Unajua, kitabu cha Waebrania ni waraka maalumu ambao mwandishi aliwaandikia **Wayahudi** waliokuwa wamemwamini Yesu, wakawa wanapitia dhiki na mateso makubwa kutoka kwa ndugu zao ambao walikuwa wanaamini **Torati pamoja na Musa** kama Nabii wao Mkuu aliyetumwa na Mungu na siyo Yesu Kristo. Soma ***Ebr.3:12-19, 4:14-16, 6:9-12, 10:19-25 na 13:20-21*** kuthibitisha kwamba waraka huu waliandikiwa Wayahudi waliokuwa wameokoka.

- Walihimizwa kutobadili msimamo hata kama wanapitia katika dhiki na mateso mbalimbali; wamwangalie Yesu (walinganishe mateso wanayoyapitia na yale aliyopitia Yesu kama yanalingana). Mwandishi alitumia sura nzima ya 11 ya Ebrania!! Kuwataja mashujaa wa imani na yote waliyoyapitia kabla ya kuwa mashujaa kwa lengo la kuwafungua ufahamu katika mashindano waliyokuwa nayo na wao.

- Hili kosa la **kutoshika** sana ungamo letu na kuwa watu wa **kugeukageuka** daima ndilo lililowagharimu sana wana wa Israeli waliokombolewa kutoka utumwani Misri. ***Kut. 14:9-14, 16:1-18, 17:1--, 32:1-6, Hes. 14:1-25 n.k***

- Ungamo letu na Yesu Kristo ni zaidi ya ungamo la ndoa; lakini watu wanaweza kustahimili mengi katika ndoa zao kuliko kustahimili mengi kwa ajili ya Kristo

  " **uvumilivu** ni kigezo muhimu sana katika kushika ungamo letu bila kugeukageuka maana kabla ya kushinda lazima tutapitia dhiki nyingi (mitihani) kama Yesu alivyotuambia. ***Yoh .16:33*** " **maana hasa ya Neno uvumilivu (Endurance)** ***2 Timoth 4:5*****. Ni uwezo anaokuwa nao mwamini ndani ya moyo wake unaomwezesha kuchukuliana na hali (mambo) magumu pasipo kulalamika (kunung'unika). Tunda hili la Roho Mtakatifu hujulikana ndani ya mwamini kutokana na jinsi alivyoitikia wakati alipokuwa anakabiliana na majaribu (mambo magumu). Mfano mzuri wa uvumilivu ni mwanamke anapokuwa mjamzito.** ***Yoh.16:20-21,*** **au mgonjwa anapotundukiwa drip.**
- Tabia hii (tunda hili) la uvumilivu linakaa ndani ya mwamini pale tu anapoamua kumtii Mungu na watumishi wake pasipo kutaka **kujitetea** au kulalamika kwa faida ya mwili huu. Mfano Ezekieli ***Ezek. 24:15-24.***

b. **Hakikisha unaweka kando kabisa mambo yatakayo kuwa mzigo kwako katika mashindano ikiwa ni pamoja na dhambi inayokuzinga kwa upesi!! All incardinate affection and concern for the body, and present life and world).** Mwandishi alitumia mfano wa mashindano ya mbio ndefu

kutaja sifa za mkimbiaji akitaka kutuonya wazi kwamba mkimbiaji mzuri ni yule anayeudhibiti mwili wake na kujizuia na desturi nyingi zisizotakiwa za ulimwengu huu. Zipo desturi za ulimwengu huu ambazo mkimbiaji wa mbio ndefu lazima aziepuke kabisa. (Leo tuko uwanjani sisi waamini tulio bado duniani tukikimbia, na mashahidi waliomaliza mbio hizo (waliolala katika Bwana) ndiyo wamekaa jukwaani wakituangalia jinsi tunavyokimbia na pengine wengi wa mashujaa hawa wanashikwa na mshangao pindi wanapotuona jinsi tunavyokimbia katika mashindano haya, lakini hawawezi tu kusema nasi!! Mashindano yetu ni ya mbio ndefu hadi Kristo atakaporudi, ukiwa na mzigo moyoni kwa vyovyote utachoka na kushindwa mashindano haya. ***1Samwl.17:38-39***. Dhambi iliyokuwa inawazinga wana wa Israeli haraka sana ni kila jaribu linapotokea **wanakumbuka kurudi Misri wanakumbuka sufuria za nyama, matango, tikiti hadi vitunguu saumu!!**. Inaonekana adui hataki kabisa tukane maisha ya kale kabla ya kuokoka wakati **Neno la Mungu linatutaka tuyakane kabisa na tuwe na mtazamo mwingine mpya katika Kristo Yesu.** ***2Kor 5:16-17*****. Hapa ndipo mahala kwa kweli panapohitaji uangalifu na hatua kali sana za Kiroho- kukana mila zetu; dini zetu, mapokeo yetu, mienendo yetu ya nyuma ya kidunia, marafiki zetu wa kidunia n.k. bila mambo haya kuwekwa kando ikiwa ni pamoja na heshima zetu. Mashindano haya yatatushinda** ***2Samwl. 9:6-8*****. Mefiboshethi alijiona kama mbwa mfu tu alipokwenda mbele za Mfalme Daudi ambaye ni mwanadamu, je sisi mbele za Yesu Mfalme wa dunia nzima kutuchagua na kutukaribisha kwake, tunakwenda kwake kama kwa shemeji au mjomba!! Tunasujudu!! Tunajitambua!!**

- Tusipokubali kuweka kando kwanza heshima zetu na mambo mengine yote ya kale na kupomoka kabisa mbele zake, ni vigumu mno kuona akijidhihirisha kwetu,na kushinda mashindano haya itakuwa ndoto tu.

c. **Mwandishi anataja siri ya tatu kwa wakiambaiji hawa kwamba wanaposhindana wamwangalie Yesu ambaye ndiye mwanzilishi wa mbio za kiroho kwa imani**
***Ebr .12:2.*** Maana yake hasa maneno haya ya kumtazama Yesu mwandishi anataka kufahamu kwa kina kwamba

i. **Yesu alijitoa kuingia katika mashindano haya kwa hiari yake mwenyewe na kwa mapenzi yake. *Ebr 10:1-10* na kamwe hakulazimishwa wala kusukumwa na chochote**

*ii.* **Alijitoa kuingia katika maombi ya kila siku pamoja n kulia sana kwa hiari yake bila kusukumwa wala kusimamiwa na mtu yeyote. *Ebr 5:7-10, Luk 22:40-43, Mark 1:35***

*iii.* **Yesu Kristo alijifunza kwa kupitia mateso; gharama ambayo inapaswa kulipwa pale mteule anapoamua kuishi maisha ya uaminifu wa kumtii Mungu katika ulimwengu huu ulioharibika.**
**(Filp *2:5-9, Isay 50: 4-9* bila kukubali kulipa gharama siyo rahisi kushinda katika mashindano haya. *Luk14:25-29, 1Nyak .21:24***

*iv.* **Yesu Kristo alidumu maisha yake yote katika kumpendeza Mungu Baba ambaye ndiye aliyekuwa chanzo cha nguvu zake na msaada wake wakati wote. *Yoh 18:4-11, Math. 26:51-56***

d. **Mwandishi anataja siri ya nne ya kipekee sana iliyomfanya Yesu asikate tamaa katika mashindano aliyokuwa nayo na dunia hii kwamba mbele yake kulikuwa na furaha kuu (heshima ya ajabu) iliyokuwa inamngoja ikiwa atashindana hadi mwisho sawasawa. *Ebr. 12:2, Filp2:9-11, Ufun 5:1-14, Ebr. 1:8-14.* Haleluya.**

- Ufahamu huu kamili wa Ki- Mungu wa kufahamu kwamba kuna furaha ya ajabu inayotungoja na sisi endapo tutashindana kwa halali mpaka mwisho ndiyo ambao tumeukosa kabisa, shetani anajitahidi usiku na mchana kupofusha fikra zetu tusilijue jambo hili kwa kina maana anafahamu fika kwamba tukilijua kama Mtume Paulo alivyolijua na upana wake, hatutakubali kamwe

kudanganywa na hivi vitu vidogo vya dunian hii. ***2Kor 4:1-4, 2Kor 12:1-16, Ufun. 21:9-27.***

- Watu wa madini wakipima eneo na kugundua ya kwamba chini sana pana madini ya dhahabu au almasi au Tanzanite n.k. watatumia gharama zote na siku nyingi hadi siku moja wayapate; Wateule katika kushindania imani hii, tukipata tu ufahamu ndani ya miyoyo yetu kabisa kwamba watakaoshinda watavikwa taji mbele za Mungu siku ile, na kwamba tutasahau taabu na kwamba tutawahukumu hadi malaika; hakuna atakayeshindana kwa mzaha wala kungojea kuhimizwa himizwa!! ***Ufun. 2:7, 10, 17 Ufun. 2:26-28, 3:5, 12.*** Bwana yafumbue macho yetu ya ndani ili tuone mambo matukufu yanayotungoja!!!

**Note**: Katika mashindano tuliyonayo ni lazima kushinda au kushindwa. Hakuna kuwa katikati!! Nitafafanua sana jambo hili katika somo lijalo. Azimia kuwa mshindi katika mashindano haya ya imani ili ujiunge na kundi kubwa la washindi walioshindania imani hii tangu Agano la Kale na hadi sasa. **Amina**

***Na***
***Askofu Dr.L.Mwizarubi***
***Octoba 2021***